**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

**Kumb. Na.KMC.R.30/11/VOL.II/62** **Tarehe: 25 Juni, 2025**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi za Ajira ya Muda ya Wakusanya Mapato nafasi Arobaini na Tisa (49).

## SIFA ZA MWOMBAJI

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe amehitimu Kidato cha IV na awe na Ufaulu wa Daraja la nne na kuendelea.
iii. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani.
iv. Awe na Mdhamini mwenye makazi yake Halmashauri ya Manispaa Kahama mwenye Mali isiyo hamishika.
v. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujituma bila kusimamiwa
vi. Awe na Umri wa kuanzia Miaka 18 hadi 35.
vii. Awe tayari kufanya kazi katika Kata yoyote ya Manispaa ya Kahama.
viii. Awe na uzoefu wa kukusanya Mapato kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja.
ix. Kipaumbele pia atapewa anayefahamu kuendesha Pikipiki.

## MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA

i. Awe na umri ya miaka 18-35 (Ambatanisha cheti cha kuzaliwa)
ii. Waombaji waambatishe vivuli vya Vyeti vyao vya Elimu na taaluma pamoja na maelezo binafsi (CV).
iii. Katika barua ya maombi, weka Namba yako ya simu inayopatikana Muda wote.
iv. Barua zibandikwe picha mbili (2) - Passport size.
v. Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili.
vi. Mwisho wa kupokea maombi ni **08/07/2025** saa **9:30** alasiri.

vii. Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472,
**KAHAMA**

Limetolewa na:

Masudi S. Kibetu
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**KAHAMA**

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA